



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Saba – Tarehe 30 Mei, 2016.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:

40. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na
Mazingira:

Bodi ya uhaulishaji Ardhi ni chombo kilichoundwa ili
kufanikisha mambo ya uhaulishaji.

- a) Je tangu ilipoundwa imeweza kuingiza mapato kiasi gani
katika mfuko wa Serikali na imeshakutana mara ngapi.
- b) Je ni utaratibu gani unaotumika wakati Bodi inapotaka
kufanya maamuzi.

WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO:

68. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID MOHAMMED DIMWA (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

ZBC TV ni chombo muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar kwa kupata habari za ndani na kimataifa.

Je, ni sababu gani inayopelekea chombo hicho kupoteza sauti na kuganda picha mara kwa mara.

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:

48. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kutokana na ukosefu wa mashine muhimu ya kukagua mizigo na abiria kumepelekea kuwepo na malalamiko kwa muda mrefu kwa wananchi kupekuliwa na askari kwa kutumia mikono na kupapaswa maungoni yakiwemo maeneo ya faragha.

- a) Mashine ya ukaguzi wa mizigo na abiria bandarini inagharimu kiasi gani mpaka Serikali ishindwe kununua mashine hiyo.
- b) Serikali haioni ni uvunjaji wa haki za binaadamu kufanya ukaguzi kwa kupapasa sehemu za viungo vya mwili wa abiria, na kupekua bila ya kujali jinsia na mzigo wa mwanamke kupekuliwa na mwanaume.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka 2016/2017.

Zanzibar,
30 Mei, 2016.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA